
# #BungeLive

Kufuatia serikali kusitisha kurushwa moja kwa moja kwa vipindi vya Bunge katika luninga, Twaweza kupitia mpango wake wa Sauti za Wananchi, wamefanya utafiti kuhusu maoni ya wananchi kufuatia hatua hii. Takwimu zifuatazo hapa chini zinatoa muhtasari wa maoni ya wananchi yanayotokana na utafiti huu wenye uwakilishi wa kitaifa unaotumia simu za mkononi. Utafiti huu unawakilisha Tanzania Bara tu. Takwimu hizi zilikusanywa mwezi Machi 2016.


### *Jambo la 1. Watanzania wanne kati ya kumi wamewahi kuangalia matangazo ya bunge ya moja kwa moja kupitia runinga.*

Watanzania wanne kati ya kumi wamewahi kuangalia matangazo ya moja kwa moja ya bunge kupitia runinga, na sita kati ya kumi wamesikiliza matangazo ya bunge ya moja kwa moja kupitia redio. Huku ikiwa ni 15% tu ya kaya Tanzania Bara zinazomiliki runinga (kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012). Ukilinganisha na wananchi waliosema wameangalia bunge kupitia runinga idadi yao ni kubwa sana.





### *Jambo la 2. Asilimia kubwa ya wananchi wameangalia au wamesikiliza vipindi vya bunge hivi karibuni.*

Zaidi ya nusu ya wananchi waliosema wameangalia ama kusikiliza vipindi vya bunge, wamefanya hivyo ndani ya miezi miwili iliyopita. Takriban robo yao wameangalia au kusikiliza bunge ndani ya mwezi mmoja uliopita, na mtu mmoja kati ya watatu amefanya hivyo ndani ya mwezi mmoja hadi miwili iliyopita. Hii inadhihirisha kuwa kuna ufuatiliaji mkubwa wa vipindi vya bunge vinavyorushwa kupitia runinga na redio.




### *Jambo la 3. Wananchi nane kati ya kumi wanapinga uamuzi wa kusitishwa kwa matangazo ya moja kwa moja ya bunge.*

Asilimia kubwa (79%) ya watanzania wanapinga vikali uamuzi wa serikali wa kusitisha matangazo ya moja kwa moja ya bunge. Huku wengi wao wakionesha "kupinga vikali" (57%; haijaoneshwa kwenye kielelezo). Suala hili limeonekana kugusa hisia za wengi, huku maamuzi haya ya serikali, yakionekana kutokuungwa mkono na wananchi.




Muhtasari huu umeandikwa na umeandaliwa na Twaweza East Africa.
Umetolewa Juni 2016

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301 | Barua Pepe: uwazi@twaweza.org
www.twaweza.org/sauti

*Kumbuka: Asilimia zinaweza zisifike 100 % kutokana na makadirio*


Sauti za Wananchi

Twaweza ni sisi

***Jambo la 4. Karibu watanzania wote wanasema ni muhimu kwa vipindi vya bunge kurushwa moja kwa moja kupitia runinga na redio.***

Walipoulizwa kama kuna umuhimu wa vipindi vya bunge kurushwa moja kwa moja kupitia runinga na radio, asilimia kubwa (92%) wamesema ni muhimu sana.


**Je unadhani kuna umuhimu wa vipindi vya Bunge kurushwa moja kwa moja kupitia Redio na Runinga?**




***Jambo la 5. Sababu kuu za kutaka matangazo ya bunge yarushwe moja kwa moja ni pamoja na kufuatilia utendaji wa wabunge pamoja na haki ya wananchi kupata habari.***

Sababu kuu iliyotolewa na karibu nusu (46%) ya wananchi wanaotaka vipindi vya bunge virushwe moja kwa moja, ni kufuatilia utendaji wa wabunge. Asilimia 44 wanasema ni muhimu kwa sababu wananchi wana haki ya kufahamu kinachoendelea bungeni. Asilimia ndogo (29%) wanasema matangazo ya moja kwa moja yalikuwa yanaaminika zaidi, kwakuwa watazamaji/wasikilizaji huona na kusikia wenyewe kile kinachoendelea. Asilimia 16 walidai kuwa inampa fursa mwananchi kupata taarifa sahihi badala ya kuzisoma kwenye magazeti, huku asilimia 16 ingine wakisema kuwa inawasaidia wananchi kufatilia mijadala ya bunge kwa wakati.

**Kuna umuhimu gani wa kurusha matangazo ya Bunge moja kwa moja kupitia redio au runinga?**




***Jambo la 6. Pamoja na kukumbushwa suala la gharama kubwa ya kurusha matangazo ya moja kwa moja, bado wananchi wanaunga mkono urushwaji huo.***

Wananchi walipoambiwa wachague moja kati ya kauli mbili kuhusu urushwaji wa moja kwa moja wa matangazo ya bunge kupitia runinga au redio, kila kauli ikiuliza kama gharama inaweza kuwa chanzo, wananchi walionyesha kutokujali suala la gharama. Asilimia 88 walisema vipindi vya bunge virushwe moja kwa moja bila kujali gharama, ukilinganisha na asilimia 12 ambao wao waliona ni muhimu suala la bajeti likazingatiwa. Vilevile, asilimia 80 wanaona matangazo ya moja kwa moja kutoka bungeni ni muhimu kama yalivyo masuala mengine, huku asilimia 20 wakisema pesa hizo zitumike kwenye huduma nyingine za jamii. Vilevile, wananchi wameunga mkono kuruhusiwa kwa vyombo vya habari vya binafsi kurusha matangazo ya bunge ya moja kwa moja iwapo serikali imeshindwa kumudu gharama.

**Chagua kauli unayokubaliana nayo zaidi:**

